



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA
MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA



TAARIFA KWA UMMA

Dodoma, Mei 08, 2024

Kufuatia mapitio ya orodha ya Taifa ya Dawa Muhimu (National Essential Medicine List - NEMLIT) yaliyofanywa na Wizara ya Afya Aprili 30, 2024 kwa kujumuisha muunganiko, muundo na nguvu kwa dawa 178 pamoja na kujumuisha dawa nne zilizokuwepo kwenye Mwongozo wa Taifa wa Matibabu lakini hazikuwemo kwenye NEMLIT na hatimaye kusaini nyongeza (addendum), Mfuko wa Bima ya Afya wa Taifa umejumuisha dawa hizo katika Kitita chake cha Mafao cha Mwaka 2023. Hatua hii inaongeza wigo wa upatikanaji wa dawa kwa wanachama kwa kuzingatia miongozo ya tiba nchini.

Kutokana na maboresho hayo, Mfuko wa Taifa Bima ya Afya unawahakikishia wanachama wake kuwa huduma za matibabu zitaendelea kupatikana katika vituo vyote vilivyojasajiliwa nchi nzima. Endapo kutakuwa na changamoto za kiutekelezaji Mfuko unashauri vituo vya kutoa huduma viwasiliane na ofisi za Mfuko kuepuka usumbufu usio wa lazima kwa wateja wao. Kwa nyongeza, iwapo mwanachama atakutana na changamoto yoyote katika upatikanaji wa huduma tafadhali asisite kuwasiliana na Mfuko kuititia Kituo cha Huduma kwa Wateja kwa kupiga simu bila malipo namba 199.

Imetolewa na;

Grace Michael

KAIMU MENEJA UHUSIANO

Jengo la NHIF Tambukareli, Barabara ya Jakaya Kikwete, S.L.P 1437, Dodoma, Simu: +255 26 2 963 888,
Barua pepe: info@nhif.or.tz, Tovuti: www.nhif.or.tz